

ZOEZI LA HUDUMA ZA KIBINGWA KWA WAGONJWA



29 Machi, 2024

UTANGULIZI

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara ilikuwa na zoezi muhimu la kutoa huduma za matibabu ya kibingwa kama ilivyo katika utaratibu wa hospitali. Huduma hizi zilitolewa kuanzia tarehe 25 hadi kufikia tarehe 29 Machi, 2024. Huduma zilizotolewa ni pamoja na;

Huduma za uchunguzi wa magonjwa ya ndani

Magonjwa haya yanajumulisha magonjwa magonjwa yote yanayomkumba binadamu kwa sehemu za mwili za ndani, magonjwa haya yanajumuisha magonjwa ya figo, magonjwa kisukari, shinikizo la damu, kiharusi na magonjwa ya moyo ikiwemo presha na magonjwa mengine yanayopelekea shida katika Mfumo wa upumuaji ikiwemo Pumu (Asthma) na mishipa ya fahamu.

Jumla ya wagonjwa waliobainika na magonjwa haya baada ya kufika kupata matibabu walikuwa 311. Madaktari bingwa waliojikita katika utoaji wa huduma kwa wagonjwa hawa walisisitiza wananchi kuwa baadhi ya magonjwa haya ikiwemo figo , shinikizo la damu na presha na magonjwa ya magonjwa haya yanaweza kupungua kabisa endapo mtu atazingatia mfumo mzuri wa maisha ikiwemo kupunguza kiwango cha chumvi katika chakula, kupunguza ulaji wa vyakula vya mafuta mengi, kuepuka msongo wa mawazo, kula mboga za kijani kibichi, kufanya mazoezi ya mwili pamoja na kuacha unywaji wa pombe na uvutaji wa sigara.

Huduma ya matibabu ya mifupa na mivunjiko



Magonjwa haya yanaweza kusababishwa na Jeraha katika mifupa na ugonjwa wa viungo ambao unapelekea viungo kuzorota na kusababisha maumivu makali. Madaktari walieleza kuwa Magonjwa haya mengi yanaweza kusababishwa na ajali za barabarani, kurithi na hitilafu katika ukuaji.

Jumla ya wagonjwa waliokutwa na matatizo ya magonjwa ya mifupa walikuwa 163 ambapo 3 walifanyiwa upasuaji Mkubwa. Madaktari wamesisitiza kuwa wananchi kujitahidi kuwahi kupata huduma stahiki katika vituo vya kutolea huduma na kusesitiza kuachana na matibabu ya mifupa kwa njia za kienyeji kwa kuwa zinasababisha athari kubwa endapo zitafayika kinyume na kupelekea madhara makubwa zaidi.

Huduma ya matibabu ya magonjwa ya wanawake na uzazi

Huduma hizi kinajumuisha magonjwa yote yanayowakumba wanawake kwa ujumla. Magonjwa haya yanaweza kuhusisha kuziba kwa mirija ya uzazi, virusi na vimelea (fangasi) uvimbe wa ndani ya tumbo na kwenye ovari, maambukizi ya bakteria na kuvu, maambukizi katika mlango wa shingo ya kikazi na mengineyo. Jumla ya wanawake waliofika kupata huduma na kukutwa na magonjwa haya walikuwa 146 na watano (5) walifanyiwa upasuaji mkubwa. Aidha madaktari bingwa wa magonjwa walisisitiza wanawake kufika katika vituo vya kutolea huduma mapema pindi waonapo dalili za tofauti katika miili, pia kuhakikisha wanapata elimu sahihi kutoka kwa watoa huduma na kuzingatia kufuata njia sahihi za uzazi wa mpango, walisistiza pia kuzingatia uzito na urefu (BMI) katika kujua nini kifanyike ili kuepuka magonjwa ya unene uliozidi ambao unaweza kupelekea wanawake kupata tatizo la kukosa uzazi.

Huduma za kibingwa za matibabu ya Sikio, Pua na Koo (ENT)

Madaktari waliotoa huduma huku wakieleza kuwa kama sehemu nyingine yoyote ya mwili wako, masikio, pua na koo zinaweza kuathiriwa na masuala mbalimbali na kudhuru afya yako na kupelekea matatizo wakati wa kulala, kumeza na usikivu. Huduma hizi zilitolewa kwa wagonjwa 124 ambapo kundi kubwa la wagonjwa walikuwa watoto. Madaktari walifanya upasuaji wa wagonjwa 3 ambapo wote wanaendelea vema. Madaktari Bingwa hao walisisitiza kuwa Baadhi ya matatizo haya ni vigumu kutambua peke yako

hivyo mgonjwa afike kumwona daktari wa masikio, pua na koo mapema ili kupata matibabu stahiki.

Huduma za upasuaji

Magonjwa yanayofanyiwa upasuaji yanajumuisha magonjwa mengi yanayokumba mwili wa binadamu ikiwemo Bawasili (haemorrhoids) –Ngiri (hernia), Mabusha(hydrocele), Mawe kwenye kibofu cha nyongo (cholelithiasis), Bandama(spleen), Vivimbe sehemu mbalimbali za mwili - Tezi rovu(goitre) -Tezi dude -Laparotomy(ies) -Mifupa -Majipu makubwa na madogo -Michaniko njia ya haja kubwa -Fistula njia ya haja kubwa - Matiti - Vidonda vya moto -Tohara kwa wanaume - Mawe kwenye kibofu cha mkojo. Wagonjwa 90 walifika kupata huduma za magonjwa haya na jumla wa wagonjwa 13 walifanyiwa upasuaji mkubwa.

HITIMISHO

Jumla ya wananchi walionufaika na matibabu haya walikuwa 1243 Hospitali itaendelea kutoa huduma hizi kwa kushirikiana na Wizara ya Afya na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa pamoja na Wadau wa Afya kuhakikisha matibabu haya ya kibingwa yanaendelea kufanyika mara kwa mara. Zoezi hili la kambi ya madaktari bingwa linatarajiwa kufanyika tena mnamo mwezi Juni, 2024.